

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**682**


**VITENDO VYA KUJIFUNZA HISABATI**

**Muda: Saa 3**

**Mwaka : 2021**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A in alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja mambo manne ambayo mtoto wa Elimu ya Awali hujifunza wakati anachunguza fedha za noti za Tanzania.
2. Andika mbinu nne anazoweza kutumia mwalimu katika kufundisha mtoto wa Elimu ya Awali dhana ya vipimo.
3. Orodhesha hatua nne za kuzingatia wakati mwalimu anafundisha dhana ya kupunguza vitu kwa mtoto wa Elimu ya Awali.
4. Eleza kwa kifupi michezo miwili inayomwezesha mtoto kujenga dhana ya kuhesabu vitu 1 hadi 10.
5. Bainisha tofauti nne zilizopo kati ya fedha aina ya sarafu na aina ya noti za kitanzania.
6. Bainisha sifa nane za kulinganisha vitu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa dhana ya vipimo kwa mtoto wa Elimu ya Awali.
7. Taja tofauti nne zilizopo kati ya lengo kuu na lengo mahsusi katika andalio la somo la Vitendo vya Kujifunza Hisabsati.
8. Eleza kwa kifupi zana nne utakazotumia kumfundishia mtoto wa Elimu ya Awali nyakati za siku.
9. Eleza umuhimu wa mwalimu kutumia vihesabio katika kumfundisha mtoto wa Elimu ya Awali kuhesabu vitu.
10. Eleza kwa ufupi umuhimu wa nyimbo katika kumfundisha mtoto wa Elimu ya Awali kuhesabu vitu.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Pendekeza hatua nne ambazo mtoto wa Elimu ya Awali anapaswa kuzipitia katika uandishi wa namba.
12. Eleza zana nne za upimaji ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kumpima mtoto wa Elimu ya Awali kuhusu shughuli ya utengenezaji wa mapambo.
13. Eleza mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa na mwalimu wakati anachagua mbinu za kufundishia vitendo vya kuongeza na kupunguza vitu.

### SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

14. Eleza umuhimu wa upimaji wa maendeleo ya mtoto katika somo la Vitendo vya Kujifunza Hisabati.
15. Kuna changamoto gani unazoweza kukumbana nazo kwa kuwaruhusu watoto wa Elimu ya Awali kwenda kukusanya zana za kufundishia na kujifunzia katika mazingira yanayozunguka shule?
16. Eleza umuhimu wa mwalimu kutumia andalio la somo la Vitendo vya Kujifunza Hisabati wakati anapofundisha darasani.